Umoja wa Mataifa

# Azimio la Milenia.

Mkutano wa Milenia
wa wakuu wa nchi wanachama
wa Umoja wa Mataifa
New York, 6-8 Septemba 2000

## UTANGULIZI:

Azimio la Milenia la Umoja wa Mataifa ni tamko mahsusi kwa karne hii. Azimio hili lilipitishwa mwishoni mwa mkutano wa milenia wa wakuu wa nchi wanachama wa Umoja huo ambao walikutana katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa mjini NEW YORK-MAREKANI kuanzia tarehe 6 hadi 8 Septemba 2000. Mkutano huo ni wa aina yake kwa sababu ni wa kwanza kukutanisha kwa mara moja wakuu wa nchi 147 pamoja na wawakilishi kutoka mataifa 191. Idadi hii inafanya azimio hilo liwe la kipekee kwa sababu linawasilisha matakwa na mahitaji ya mataifa masikini na matajiri.

Azimio hilo la Milenia ni hitimisho baada ya mazungumzo yaliyofanyika kwa miezi kadhaa na kutilia maanani mapendekezo yaliyotolewa katika vikao vya ngazi mbali mbali. Cha maana zaidi ni kwamba nafurahi kuona kuwa mapendekezo niliyoyatoa katika ripoti yangu ya Milenia yamejumuishwa katika azimio hilo.

Madhumuni ya kuitisha mkutano huo wa Milenia yalikuwa ni kudhihirisha umuhimu wa kipindi hiki katika kuitikia wito wa kukidhi mahitaji ya binadamu. Nimesikiliza viongozi mbali mbali wa dunia wakizungumza na nikapitia azimio hili walilopitisha na nikasisimka na jinsi walivyoeleza changamoto kuu zinazowakabili na umuhimu wa kukabiliana na changamoto hizo haraka iwezekanavyo.

Viongozi hao wamejiwekea muda maalumu wa kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu fukara duniani, kuhakikisha watu wanapata maji safi na salama, kuhakikisha watoto wote bila kujali jinsia yao wanapata elimu ya msingi, kupunguza maambukizo mapya ya virusi vya UKIMWI pamoja na malengo mengine yenye kuleta maendeleo ya binadamu.

Sambamba na hilo, katika azimio hilo la Milenia la Umoja wa Mataifa, viongozi hao walioshiriki katika mkutano huo

wa siku tatu wamependekeza kuimarishwa kwa huduma za kulinda amani zitolewazo na Umoja wa Mataifa ili watu wanaokuwa katika migogoro waweze kuutegemea umoja huo. Vile wameshauri vitendo vya uhalifu, ukiukwaji wa haki, kutokuwepo kwa usawa, ugaidi na suala la kuhifadhi dunia tunayoishi kwa faida ya vizazi vijavyo yapewe kipaumbele.

Wakuu hao wa nchi na serikali pamoja na wawakilishi, vile vile wamezungumzia umuhimu wa Umoja wa Mataifa kama chombo cha watu kiweze kubadilika kulingana na mazingira ya sasa ili kitekeleze majukumu yake ipasavyo. Hapa ina maana kuwa chombo hiki kiwe na uwezo wa kutekeleza majukumu yake na matokeo yaweze kuonekana. Kwa upande wangu mimi binafsi pamoja na watumishi wangu, tunajitoa mhanga kuhakikisha kuwa Umoja wa Mataifa unafanya kazi yake kwa mujibu wa mamlaka yake. Hata hivyo, viongozi hao ni lazima wafahamu kuwa wao ndio Umoja wa Mataifa. Umoja wa Mataifa unategemea zaidi nchi wanachama wake ambao viongozi wao ndio wametoa ombi hilo.

Umoja wa Mataifa unategemea zaidi nguvu na uwajibikaji wao ili uweze kutimiza wajibu wake na uweze kuendelea kuwepo kwa faida ya wanachama wake wote. Kwao wao, na serikali zao pamoja na wananchi wao, ninaloweza kusema kuwa ni jukumu lao kuhakikisha kuwa Umoja wa Mataifa unazikabili changamoto hizo.

Kofi A. Annan
Katibu Mkuu, Umoja wa Mataifa

*Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa limepitisha Azimio lifuatalo:*

# Azimio la Milenia la Umoja wa Mataifa

## I UMUHIMU NA MISINGI:

1. Sisi wakuu wa nchi na serikali tumekutana katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa mjini NEW YORK, MAREKANI katika mwanzo wa Milenia hii ya TATU kuanzia tarehe SITA hadi NANE Septemba mwaka huu tunasisitiza tena imani yetu kwa Umoja wa Mataifa kuwa ni chombo muhimu na chenye misingi bora ya kuleta amani na maendeleo katika dunia yenye usawa.

2. Tunatambua kuwa sambamba na majukumu yetu binafsi katika nchi zetu, kwa pamoja tunawajibika kulinda na kutetea misingi ya haki, usawa, heshima na utu wa kila binadamu katika ngazi zote duniani kote. Kwa hiyo kama viongozi tunawajibika kwa binadamu wote duniani wakiwemo masikini, hususan watoto ambao mategemeo ya dunia hii yamo mikononi mwao.

3. Tunasisitiza tena imani yetu juu ya madhumuni ya Umoja wa Mataifa kama yalivyoainishwa katika Katiba yake na kwamba madhumuni na malengo hayo hayajapitwa na wakati na yana lenga dunia nzima. Ni wazi kuwa madhumuni na malengo hayo yanazidi kuongezeka umuhimu wake siku hadi siku na kupelekea mataifa na binadamu kutoka pande zote za dunia kuzidi kushirikiana na kutegemeana.

4. Tunajitoa mhanga kuhakikisha kunawepo amani ya kudumu duniani kote kwa kuzingatia madhumuni na misingi ya katiba ya Umoja wa Mataifa. Vile vile tunaunga mkono jitihada zote za kulinda utaifa wa kila

nchi na kuheshimu mipaka na uhuru wa nchi hizo sambamba na kuheshimu maazimio mbali mbali ya Umoja wa Mataifa yanayolenga kutafuta suluhisho la migogoro kwa njia ya amani na kwa kuzingatia haki na sheria za kimataifa.

5. Tunaamini kuwa changamoto kuu iliyo mbele yetu hivi sasa ni kufanya utandawazi kuwa na faida kwa watu wote, masikini na tajiri. Utandawazi una manufaa makubwa hivi sasa, lakini wanaonufaika ni wachache. Tunatambua kuwa nchi zinazoendelea na zile ambazo ziko mbioni kuendelea zina vikwazo vingi vinavyozisababisha zisinufaike na mfumo huo wa sasa duniani. Utandawazi unaweza kuwa na manufaa kwa wote pale ambapo tutaweka jitihada za pamoja zitakazozingatia tofauti zetu. Nchi changa lazima zishiriki katika jitihada hizo za kimataifa zitakazojumuisha sera na hatua zinazofanana na mahitaji ya nchi changa.

6. Tunafikiria kuwa iko misingi ambayo ni muhimu katika ushirikiano wa kimataifa hususan katika karne hii ya 21. Misingi hiyo ni pamoja na:
   - **Uhuru-** Wanawake na Wanaume wana haki ya kuishi na kutunza watoto wao katika mazingira yenye heshima ambayo hayana njaa na yasiyokiuka haki za binadamu pamoja na vitendo vya unyanyasaji. Serikali zinazochaguliwa na kushirikisha wananchi mara nyingi huwapatia wananchi wake haki hizo.
   - **Usawa-** Hakuna mtu au taifa lolote ambalo litanyimwa nafasi ya kufaidi maendeleo ya nchi yake. Ni wajibu wa kila mwanamke na mwanaume kuhakikishiwa kuwa anapata haki sawa na nafasi ya kushiriki katika shughuli za maendeleo.
   - Mshikamano-Mataifa masikini na tajiri duniani, ni lazima yagawane athari ya changamoto zinazoikabili dunia hivi sasa. Hatua hii itazingatia misingi ya kidemokrasia na usawa wa jamii. Mataifa ambayo hayanufaiki na maendeleo yoyote yale duniani ni lazima yasaidiwe.

- **Uvumilivu-** Kila binadamu anapaswa kumheshimu binadamu mwenzake bila ya kujali tofauti zao. Tofauti zozote ndani ya jamii au kati ya jamii kamwe zisipuuzwe au zisionekane kuwa ni tishio bali zitambuliwe na kuthaminiwa. Tabia ya kuwepo kwa amani na uelewano baina ya jamii zote ni lazima ipewe kipaumbele.
- **Kulinda mazingira-** Ili kuleta maendeleo endelevu, ni lazima kuwa waangalifu katika udhibiti wa mazingira na viumbe vyote hai. Hii ndiyo njia pekee itakayohakikisha kuwa utajiri wa maliasili tulizonazo hapa duniani zinatunzwa kwa faida ya vizazi vijavyo. Mfumo wa sasa wa kutumia maliasili hizi ni lazima ubadilishwe kwa faida ya vizazi vyetu vijavyo.
- Kuwajibika kwa pamoja- Jukumu la kuendeleza dunia yetu kiuchumi na kijamii ni letu wote. Sote tunawajibika kuyalinda makazi yetu dhidi ya mambo yote yanayotishia amani. Umoja wa Mataifa kama chombo chenye idadi kubwa ya wanachama ni lazima ibebe jukumu la pekee la kuhakikisha yote hayo yanatimizwa.

7. Katika kuhakikisha haya malengo tuliyojiwekea pamoja yanatekelezwa kwa mafanikio makubwa, tumeainisha malengo ambayo tumeyapa umuhimu wa pekee.

## II: AMANI, ULINZI NA KUONDOA MATUMIZI YA SILAHA.

8. Tutatumia uwezo wetu wote kuepusha watu wetu dhidi ya vita ndani ya nchi au kati ya nchi na nchi. Vita vimeua zaidi ya watu Milioni TANO katika miaka 10 iliyopita. Sambamba na hilo tutatafuta njia kutokomeza athari zitokanazo na matumizi ya silaha nzito.
9. Kwa mantiki hiyo, sote kwa pamoja tunaazimia:
   - Kuimarisha suala la kuheshimu utawala wa kisheria katika ngazi za kimataifa kama ilivyo katika ngazi ya taifa, hususan kuhakikisha nchi

wanachama wa Umoja wa Mataifa zinakubaliana na maamuzi yanayotolewa na Mahakama ya Kimataifa kwa mujibu wa katiba ya Umoja wa Mataifa, iwapo nchi zinazohusika na mgogoro husika ni wanachama wa Umoja huo.

- Kuupatia Umoja wa Mataifa uwezo wa vifaa na kifedha ili uweze kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kujenga amani na usalama duniani kuzuia migogoro au kuitatua kwa njia za amani, kulinda amani sehemu zenye migogoro na kusaidia kujenga amani katika nchi zilizokuwepo katika migogoro Kwa mantiki hiyo tunazingatia mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti ya timu ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa iliyowasilishwa katika kikao hiki cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.
- Kuimarisha uhusiano kati ya Umoja wa Mataifa na vikundi vingine vya ushirikiano baina ya mataifa kwa mujibu wa kifungu cha VIII cha Katiba ya Umoja wa Mataifa.
- Kuhakikisha nchi wanachama zinatekeleza mikataba mbali mbali ya Umoja wa Mataifa, hususan ile inayohusu udhibiti wa matumizi ya silaha, sheria za kimataifa kuhusu haki za binadamu pamoja na kushinikiza nchi wanachama kutia saini mkataba wa ROME kuanzisha mahakama ya kimataifa ya wahalifu.
- Kuimarisha jitihada za pamoja za kupiga vita ugaidi wa kimataifa na kuhakikisha kila nchi mwanachama inatia saini mikataba inayopinga vitendo hivyo.
- Kuongeza maradufu jitihada zetu za kupambana na tatizo la madawa ya kulevya duniani.
- Kuimarisha jitihada zetu za kupiga vita vitendo vya kihalifu ikiwemo biashara haramu ya fedha na ya binadamu.
- Kuhakikisha vikwazo vya kiuchumi dhidi ya mataifa kadhaa vinavyowekwa na Umoja wa

Mataifa haviathiri wananchi wasio na hatia. Kwa mantiki hiyo kutathmini mara kwa mara vikwazo hivyo ili visiweze kuathiri vibaya pande zisizohusika.

- Kuongeza jitihada za kutokomeza matumizi ya silaha kali kama vile za nyuklia kwa kutumia mikakati mbali mbali ikiwemo kuitisha mikutano ya kimataifa itakayopendekeza mbinu za kutekeleza suala hili.
- Kuunganisha jitihada zetu kutokomeza usafirishaji haramu ya silaha ndogo na silaha nyepesi hususan kwa kufanya suala la usafirishaji wa silaha liwe la wazi na liende sambamba na mikakati ya kila kanda ya kukabiliana na utumiaji hovyo wa silaha. Hatua hii izingitie vile vile mapendekezo yatakayotolewa katika mkutano uhao wa Umoja wa Mataifa kuhusu silala ndogo na silaha nyepesi.
- Kuzikumbusha nchi zote wanachama kuzingatia suala la kutia saini mkataba wa kimataifa unaozuia matumizi, utunzaji, utengenezaji na usafirishaji wa mabomu yanayotegwa ardhini, ambao pia unazungumzia suala la kuharibu silaha hizo. Sambamba na mkataba huo ni sheria ndogo zilizopitishwa na Umoja wa Mataifa kuhusiana na silaha.

10. Tunaziomba nchi zote wanachama kuendeleza amani na uelewano ndani ya nchi zao na baina ya mataifa yao kupitia michezo ya Olimpiki.

## III: Maendeleo na kupiga vita umaskini.

11. Tutatumia uwezo wetu wote kuwakomboa zaidi ya watu Bilioni moja wakiwemo wanawake, wanaume na watoto ambao wanaishi katika umaskini uliokithiri. Tumejizatiti kuhakikisha haki ya kila mtu kuendelea inageuka na kuwa ya kweli ili kila binadamu aweze kupata mahitaji yake muhimu.

12. Kwa mantiki hiyo basi, tunaazimia kujenga mazingira katika ngazi ya kitaifa na kimataifa yatakayowezesha binadamu kushiriki katika shughuli za maendeleo na hivyo kuutokomeza umaskini.

13. Mafanikio ya mkakati huo, hata hivyo yanategemea zaidi utawala bora katika kila serikali na katika ngazi ya kimataifa ambapo pia suala la uwazi katika matumizi ya fedha na mfumo wa biashara ni lazima uangaliwe. Tumejizatiti kuhakikisha kuwa mfumo wa fedha na biashara duniani unakuwa wa usawa, unafuata sheria na kamwe hauwi wa kibaguzi.

14. Tuna wasiwasi juu ya vikwazo ambavyo nchi zinazoendelea zinakumbana navyo katika kutafuta fedha zinazohitajika kwa maendeleo endelevu. Hata hivyo basi tutahakikisha mkutano wa kimataifa juu ya fedha na maendeleo utakaofanyika mwaka 2001 unakuwa wa mafanikio makubwa.

15. Sambamba na hilo tuko mstari wa mbele kushughulikia mahitaji ya kipekee ya nchi changa. Kwa mantiki hiyo tunaunga mkono mkutano wa TATU wa nchi changa ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa ambao utafanyika mwezi Mei mwaka 2001, na tutajitahidi kuufanikisha. Kwa hivyo basi, tunazitaka nchi tajiri kuzingatia yafuatayo:

- Wakati utakapokuwa unafanyika mkutano huo, ziwe zimepitisha sera zinazoondoa ushuru wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nchi changa.
- Kutekeleza mpango wa kuzifutia madeni nchi masikini kabisa duniani zenye madeni makubwa hususan zile ambazo zitakuwa zimeandaa mikakati kama dalili ya kuwa tayari kutokomeza umaskini miongoni mwa wananchi wao.
- Kutoa misaada zaidi kwa nchi maskini ambazo zinaonyesha jitihada za kutumia misaada hiyo katika kuondoa umaskini.

16. Tumejizatiti kutumia mbinu mbali mbali katika ngazi za kitaifa na kimataifa ili kushughulikia madeni yanayozikabili nchi zenye kipato cha chini na kipato cha kati. Hatua hii itawezesha nchi hizo ziweze kulipa madeni yao.

17. Vile vile tutashughulikia suala la mahitaji muhimu ya visiwa vidogo ambavyo ni miongoni mwa nchi zinazoendelea. Utekelezaji wa suala hili utazingatia Mpango wa Utekelezaji wa BARBADOS na maazimio ya kikao maalum cha 22 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Tunaiomba Jumuiya ya Kimataifa kuhakikisha kuwa katika kuweka orodha ya mataifa ambayo yako katika hatari ya kuathirika na umaskini, mahitaij ya visiwa vidogo ambavyo ni miongoni mwa nchi zinazoendelea ni lazima yatiliwe maanani.

18. Tunatambua mahitaji ya kipekee ya nchi ambazo hazina bandari. Kwa mantiki hiyo basi tunaomba wahisani wa kitaifa na kimataifa kuongeza misaada yao ya kiufundi kwa nchi hizi ili ziweze kuboresha mifumo yao ya usafirishaji ili ukosefu wa bandari usiwe kikwazo cha maendeleo yao.

19. Tunaazimia vile vile:

- Ifikapo mwaka 2015, kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu maskini ambao kipato chao ni chini ya dola moja kwa siku na vile vile kupunguza kwa kiasi hicho hicho idadi ya watu wanaokumbwa na njaa na wale wanaoshindwa kupata maji safi na salama.
- Katika kipindi hicho hicho cha miaka 15 ijayo, kuhakikisha watoto wote wa kike na wa kiume wanakuwa na uwezo wa kumaliza shule ya msingi na kwamba watoto wote hao, wa kike na wa kiume wanapata fursa sawa ya kwenda shuleni.
- Kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2015 idadi ya vifo vya wanawake wajawazito vinapungua kutoka kiwango cha sasa kwa asilimia 75 wakati vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano

vipungue kwa theluthi mbili kutoka kiwango cha sasa.

- Ifikapo mwaka huo huo, kuhakikisha maambukizo mapya ya virusi vya UKIMWI pamoja na UKIMWI yanakuwa yamepungua na kwamba iwepo mikakati mahsusi ya kukabiliana na magonjwa kama MALARIA ambayo ni tishio kwa uhai wa binadamu.
- Kutoa msaada maalum kwa watoto ambao wazazi wao wamefariki dunia kutokana na UKIMWI.
- Ifikapo mwaka 2020 tuwe tumefikia lengo letu la kuboresha maisha ya watu wapatao Milioni-100 wanaoishi katika makazi yasiyo na hadhi kama ilivyobainishwa katika mkakati wa MIJI BILA MAKAZI MACHAFU.

20 Vile vile tunaazimia:

- Kuendeleza usawa wa kijinsia na kuwapa wanawake uwezo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii kama njia pekee ya kutokomeza njaa, umaskini na magonjwa, na hatimaye kuleta maendeleo ambayo ni endelevu.
- Kuendeleza mikakati inayotoa fursa na uwezo kwa vijana popote pale walipo kuwa na nafasi ya kufanya kazi ya uzalishaji na yenye hadhi.
- Kutoa hamasa kwa viwanda vya madawa ulimwenguni kuhakikisha madawa muhimu yanapatikana na kwa bei nafuu ambayo itawezesha nchi maskini kuzinunua kwa mahitaji ya wananchi wake.
- Kuendeleza ushirikiano wa hali ya juu na sekta binafsi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kama njia moja ya kuleta maendeleo na kupiga vita umaskini.
- Kuhakikisha kuwa manufaa yatokanayo na maendeleo ya sayansi na teknolonia hususan katika sekta ya mawasiliano yanafikia binadamu wote kwa mujibu wa mapendekezo yaliyomo kwenye

Azimio la mkutano wa mawaziri wa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa-ECOSOC-2000.

## IV: KULINDA MAZINGIRA YETU

22. Tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kuwa hakuna binadamu yeyote yule, wakiwemo watoto wetu na wajukuu wetu ambao wataishi katika sayari ambayo imeharibiwa na kuchafuliwa kutokana na shughuli za binadamu kwa kiasi kwamba hakutakuwepo na rasilimali za kutosheleza mahitaji yao.
23. Tunarudia tena azma yetu ya kuunga mkono misingi yote ya maendeleo endelevu ikiwemo ile iliyobainishwa kwenye ajenda 21 ambayo ilikubaliwa kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira na Maendeleo.
24. Kwa mantiki hiyo tutabuni mikakati mipya ya udhibiti na usimamizi wa mazingira, na kwa kuanzia tutatekeleza yafuatayo:
    - Tutajitahidi ili mkataba wa KYOTO kuhusu mazingira uanze kutumika ifikapo mwaka 2002, kipindi ambacho ni miaka 10 tangu kufanyika kwa mkutano wa kimataifa wa Mazingira na Maendeleo, na kwa hatua hiyo kuanza kutekeleza suala la kupunguza matumizi ya gesi/hewa zinazoharibu mazingira.
    - Kuongeza nguvu na kuunganisha jitihada zetu katika kuhifadhi, kulinda na kuendeleza aina zote za misitu.
    - Kushinikiza kutekelezwa ipasavyo kwa mikataba mbali mbali ya kuhifadhi mazingira hususan ule wa Bionuwai na ule wa kuzuia dunia kugeuka jangwa hasa katika nchi za AFRIKA ambazo zinakabiliwa na ukame au kugeuka jangwa.
    - Kupiga marufuku matumizi mabaya ya maliasili za majini kwa kuweka mikakati ya matumizi

mazuri ya maliasili hizo kuanzia ngazi za kaya, kitaifa na kimataifa, mikakati ambayo itahakikisha matumizi sawa ya maliasili hizo.

- Kuongeza ushirikiano baina yetu ili kupunguza idadi na athari mbaya zitokanazo na majanga yasiyoweza kuzuilika na yale yanayosababishwa na binadamu.
- Kuhakikisha taarifa kuhusu teknolojia ya matumizi ya chembechembe za urithi katika miili ya wanyama zinapatikana kwa watu wote.

## V: HAKI ZA BINADAMU, DEMOKRASIA NA UTAWALA BORA.

25. Tutatumia uwezo wetu wote kuendeleza demokrasia na kuimarisha utawala wa sheria pamoja na kuheshimu haki zote za msingi za binadamu ikiwemo haki ya maendeleo.

Kwa hiyo, tunaazimia:

- Kuheshimu na kuunga mkono Mkataba wa kimataifa wa haki za binadamu.
- Kujitahidi kulinda kwa nguvu zote na kuendeleza katika nchi zote haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.
- Kuimarisha uwezo wa mataifa yote kutekeleza misingi ya kidemokrasia na kuheshimu haki za binadamu wote zikiwemo haki za makabila madogo.
- Kupiga vita aina zote za unyanyasaji dhidi ya wanawake na kutekeleza mkataba wa kimataifa wa kupiga vita aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake-CEDAW.
- Kuchukua hatua mahsusi kuhakikisha haki za binadamu wakiwemo wahamiaji pamoja na wafanyakazi wahamiaji na familia zao zinalindwa na kutokomeza ubaguzi wa rangi katika jamii zote huku tukijenga tabia ya kuvumiliana mion-

goni mwa jamii bila kujali tofauti zilizopo.

- Kufanya kazi kwa ushirikiano zaidi hususan katika ngazi ya kisiasa na kutoa fursa zaidi kwa wananchi kushiriki katika mfumo wa utawala.
- Kuhakikisha vyombo vya habari vinakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yao ya kutoa habari kwa jamii na vile vile jamii kuwa na haki na uwezo wa kupata habari.

## I: KUWALINDA WALIO KATIKA HATARI

26. Tutatumia uwezo wetu wote kuhakikisha kuwa watoto pamoja na raia wote ambao wameathirikana majanga kama vile migororo ya kivita, mafuriko na mauaji ya halaiki pamoja na matatizo mengine ya dharura ya kibinadamu wanapata kila msaada unaohitajika ili hatimaye waweze kurejea katika maisha yao ya kawaida.

Ili kutekeleza jambo hilo, tunaazimia:

- Kupanua na kuimarisha uwezo wetu wa kuwalinda raia walio katika matatizo ambamo mazingira yake ni magumu. Tutafanya hilo kwa kuzingatia sheria za kimataifa za masuala ya kibinadamu.
- Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa ikiwemo kusaidiana katika matatizo yoyote yanayotokea, kuratibu shughuli za kutoa misaada ya dharura na kuwasaidia wakimbizi na watu wote walioyakimbia makazi yao kurejea makwao bila kushinikizwa na kuungana na familia zao na kuishi maisha yenye heshima na hadhi.
- Kuhamasisha nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuridhia na kuanza kutekeleza kikamilifu mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto-CRC-pamoja na nyongeza za mkataba huo ambazo zinapiga vita watoto kushiriki katika migogoro ya kivita, biashara ya watoto na watoto kushiriki katika vitendo vya ukahaba na upigaji wa picha cha uchi.

## VII: KUTILIA MAANANI MAHITAJI PEKEE YA AFRIKA

27. Tutaunga mkono jitihada za AFRIKA za kujenga demokrasia pamoja na kusawaidia waafrika katika jitihada zao za kuleta amani ya kudumu, kupiga vita umaskini na kuleta maendeleo endelevu ili bara hilo liwe mshiriki mkamilifu katika uchumi wa dunia.

28. Kwa mantiki hiyo tunaazimia:
    - Kutoa msaada wa kutosha kwa taasisi za kisiasa za nchi zenye demokrasia changa barani AFRIKA.
    - Kuimarisha jitihada za AFRIKA za kuzuia kuibuka kwa migogoro barani humo kwa kuunga mkono taasisi za kikanda zilizomo barani humo za kuzuia migogoro na kuhakikisha kunakuwepo na rasilimali za kutosha kusaidia shughuli za kulinda amani barani AFRIKA.
    - Kuchukua hatua mahsusi za kusaidia AFRIKA kukabiliana na changamoto ya kupiga vita umaskini na kujiletea maendeleo endelevu. Tutafanya hivyo kwa kusisitiza suala la nchi za AFRIKA kufutiwa madeni, kuhakikisha nchi hizo zinapata soko la bidhaa zao, kuongeza misaada na vitega uchumi pamoja na kuhakikisha nchi za AFRIKA zinapata teknolojia ya kisasa.
    - Kusaidia AFRIKA inajenga uwezo wake wa kupambana na maambukizo ya virusi vya UKIMWI pamoja na magonjwa mengine ya kuambukiza.

## VIII. KUIMARISHA UMOJA WA MATAIFA.

29. Tutafanya kila jitihada kuhakikisha Umoja wa Mataifa unakuwa chombo chenye uwezo kuhakikisha masuala yote tuliyoyapa kipaumbele yanatekelezwa: Kuhakikisha binadamu wote duniani wanapata fursa ya kujiendeleza; kupiga vita umaskini, magonjwa na maradhi; kupiga vita ukiukwaji wa sheria,

unyanyasaji wa aina yoyote ile, ugaidi na uhalifu pamoja na uharibifu wa mazingira ambamo tunaishi.

30. Kwa mantiki hiyo tunaazimia:

- Kusisitiza tena kuwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ni chombo kikuu cha kupitisha maamuzi, kupitisha sera na kwamba ndicho chenye uwakilishi mkubwa unaokiwezesha kutekeleza majukumu hayo ipasavyo.
- Kuongeza jitihada zetu kuharakisha urekebishaji wa mfumo wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.
- Kuimarisha Baraza la Uchumi na Kijamii la Umoja wa mataifa -ECOSOC-kwa kuzingatia mafanikio yake na kuliwezesha Baraza hilo kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa katiba ya Umoja wa Mataifa.
- Kuimarisha mahakama ya Kimataifa ili iweze kuhakikisha sheria na haki inakuwepo katika masuala ya kimataifa.
- Kuhamasisha kuwepo kwa ushirikiano na uratibu miongoni mwa vyombo vyote vikuu vya Umoja wa Mataifa ili viweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
- Kuhakikisha Umoja wa Mataifa unapatiwa kwa wakati muafaka rasilimali zinazotakiwa ili uweze kutekeleza majukumu yake.
- Kuishawishi sekretarieti ya Umoja wa Mataifa kutumia rasilimali zilizopo kwa uangalifu na kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa faida ya nchi wanachama.
- Kuhakikisha Mkataba wa kimataifa juu ya usalama wa Umoja wa Mataifa pamoja na watumishi wake unazingatiwa.
- Kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano mzuri wa kisera baina ya mashirika ya Umoja wa

Mataifa, taasisi za BRETTON WOODS na Shirika la Biashara duniani-WTO na taasisi zingine za kimataifa kwa lengo la kuratibu kwa pamoja shughuli za amani na maendeleo duniani.

- Kuimarisha ushirikiano zaidi kati ya Umoja wa Mataifa na mabunge ya nchi wanachama wa Umoja huo kupitia Umoja wa Mabunge duniani. Ushirikiano huo uwe katika sekta za amani na usalama, maendeleo ya Uchumi na Kijamii, sheria za kimataifa, haki za binadamu, demokrasia na masuala ya kijinsia.
- Kutoa fursa zaidi kwa sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii katika kuchangia kufanikiwa kwa malengo na mipango ya Umoja wa Mataifa.

31. Tunaliomba Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kupitia mara kwa mara utekelezaji wa vipengele vya Azimio hili la Milenia kwa kumuagiza Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuandaa ripoti ya utekelezaji itakayokuwa inawasilishwa kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

32. Tunasisitiza tena katika mkutano huo wa historia kuwa Umoja wa Mataifa ni chombo ambacho kinahitajika zaidi hivi sasa kuliko wakati wowote ule kwa lengo la kujenga amani duniani, kuleta ushirikiano na maendeleo. Kwa mantiki hiyo basi tunaahidi kuendelea kutoa msaada wetu kufanikisha utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea.

Azimio A/RES/55/2
8 Septemba 2000

Imechapishwa na Idara ya Habari ya Umoja wa Mataifa (DPI)
DPI/2163 - September 2000 - 10m